

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 37 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** MACHI 2024

SERIKALI YAAHIDI KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA KIUTUMISHI ZA WALIMU WOTE NCHINI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akifungua kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichofanyika Februari 3, 2024 jijini Dodoma kwa lengo la kuhakiki kwa kina changamoto za walimu.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

KONGOLE KWA SERIKALI KWA KUWEKA NGUVU KATIKA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Katika kuhakikisha kila mwalimu mwenye malalamiko halali hususan juu ya masuala ya kucheleweshwa kupanda cheo anapata haki yake, Serikali imeingia katika hatua nyingine ya uhakiki wa taarifa za walimu.

Itakumbukwa kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilifanya uhakiki wa awali ambapo hivi karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) alikaririwa akisema Serikali imejipanga kutatua changamoto hizo za walimu.

Baada ya hatua hiyo, Serikali imekwenda mbali zaidi ambapo mapema mwezi Februari, 2024 kilifanyika kikao kazi kilichowakutanisha maafisa kutoka Ofisi ya Rais UTUMISHI, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TSC

na Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote nchini kwa lengo kufanya uhakiki wa kina kwa kuhusisha taarifa za watumishi zilizo kwenye Mfumo wa Taarifa za kiutumishi na Mishahara (HCMIS).

Tunaipongeza Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka uzito mkubwa katika kushughulikia maslahi ya walimu. Ni wazi kuwa changamoto za walimu zinapotatuliwa, walimu wanapata ari ya kuongeza kasi ya kutoa huduma kwa wanafunzi.

Matumaini yetu ni kuwa, baada ya zoezi la uhakiki wa taarifa hizo kukamilika, kila mwalimu mwenye madai atapatiwa haki yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Gerard J. Chami


Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**

SERIKALI YAAHIDI KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA KIUTUMISHI ZA WALIMU WOTE NCHINI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa amefungua kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali wanaohakiki kwa kina changamoto za walimu hususan upandishwaji wa vyeo.

Akifungua kikao kazi hicho Februari 3, 2024 jijini Dodoma, Waziri Mchengerwa alisema katika kuhakikisha kuwa malalamiko ya Walimu yanashughulikiwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais UTUMISHI iliagiza Tume ya Utumishi wa Walimu kufanya uchambuzi na kubaini walimu wote wenye changamoto katika upandaji wao wa vyeo.

"Niwapongeze Watendaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kubaini walimu wenye



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde akizungumza wakati wa kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichofanyika Februari 3, 2024 jijini Dodoma kwa lengo la kuhakiki kwa kina changamoto za walimu.

changamoto.

pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa malalamiko ya walimu wote yanashughulikiwa kwa ufanisi, nimeelekeza uhakiki wa kina

ufanyike kwa kuhusisha taarifa za watumishi kama zilivyo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara" amesema

Ameagiza kushughulikia kikamilifu changamoto hizo ndani ya siku 14 na kufanya kazi hiyo kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuhakikisha hakuna Mwalimu anayeachwa baada ya zoezi hilo kufanyika.

Wakati huohuo, Waziri Mchengerwa amewakumbusha Waajiri na Mamlaka zote zinazohudumia Walimu kusimamia vyema maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kutatua kero walizo nazo.

"Naomba niweke wazi mimi sitamvumilia mtendaji yeyote ambaye hawajibiki kushughulikia kero za walimu na vilevile sitamani kusikia walimu wana malalamiko kuhusu maslahi yao ya kiutumishi," amesema.



Washiriki wa kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichofanyika Februari 3, 2024 jijini Dodoma kwa lengo la kuhakiki kwa kina changamoto za walimu



Washiriki wa kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichofanyika Februari 3, 2024 jijini Dodoma kwa lengo la kuhakiki kwa kina changamoto za walimu



'MICHANGO HOLELA SHULENI HAIRUHUSIWI' – WAZIRI MKUU



Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, amesema msimamo wa Serikali umebaki vilevile kutoruhusu

michango holela inayoendeshwa kwenye shule mbalimbali nchini.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo hivi karibuni Bungeni Jijini Dodoma wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa papo yanayoulizwa na Wabunge kwa Waziri Mkuu.

Alisema michango inayoruhusiwa ni ile ya maendeleo

ambayo pia huchangiwa baada ya kamati ya shule kukaa na kukubaliana na Wananchi wa eneo husika ambapo mwenye idhini na dhamana ya kuanza kuchangisha michango hiyo ni Mkuu wa Wilaya wa eneo hilo.

"Tunaposema michango holela tunajua ipo michango inayokubalika ndani ya jamii. Michango ya maendeleo ndio inayokubalika. Mfano choo kimebomoka na gharama zake labda ni shilingi milioni mbili, Kamati ya Shule inakutana wanasema tunataka choo ili watoto wetu wapate huduma kwa wakati badala ya kusubiri kuandika barua, bajeti zipangwe mpaka huko TAMISEMI ila wao wanaweza kukubaliana hapa tuchangie mia tanotano, na mchango unaenda kwenye ujenzi au ukarabati wa choo." Alisema Waziri Mkuu Majaliwa.

Alisema pamoja na michango hiyo kuruhusiwa kwa utaratibu ulioainishwa, bado maamuzi yake yamedhibitiwa kidogo na Serikali, pamoja na maamuzi ya Kamati za Shule na Kijiji kwa ajili ya maendeleo kuruhusiwa bado mwenye mamlaka na idhini ya kuanza kuchangisha ni Mkuu wa Wilaya jambo lililokusudiwa na Serikali kuondosha watu kukaa na kutengeneza michango isiyokubalika.

"Kwahiyo msimamo wa Serikali bado ni uleule kwamba hatuhitaji michango holela, michango holela ni ile mtu mmoja anakurupuka anasema kesho kila mmoja aje na shilingi mia mbili ambazo hazina maelekezo yoyote. Michango ya hivi haikubaliki na tumeagiza kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kusimamia kutokuwepo kwa michango holela inayokwaza Wazazi na Walezi." Alisema Mheshimiwa Waziri Mkuu.

TRILIONI 1.29 ZATUMIKA KUBORESHA MAZINGIRA YA ELIMU – WAZIRI MKUU

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka miwili imetumia shilingi Trilioni 1.29 kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Alisema kati ya fedha hizo shilingi bilioni 454.3 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Shule za Elimu ya Awali na Msingi ambapo jumla ya Shule Mpya zilizojengwa ni 342, Vyumba vya Madarasa 9,189, Nyumba za Walimu 346, Mabweni 28 na Ukarabati wa Shule Kongwe 45.

Alisema hayo Bungeni Jijini Dodoma hivi karibuni wakati akiwasilisha taarifa kuhusu Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu ngazi ya Elimu Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Alisema utekelezaji wa mtaala mpya umeanza katika ngazi ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi - Darasa la I na III, Elimu ya Sekondari Kidato cha Kwanza katika baadhi ya fani za amali katika shule 96 za Serikali na Binafsi ambazo zina miundombinu wezeshi kama karakana na Walimu wa fani hizo.



WATAALAM WA ELIMU KUTOKA ZANZIBAR WATEMBELEA TSC KUJIFUNZA NAMNA INAVYOFANYA KAZI

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Wataalam kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Februari 12, 2024 wametembelea Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa lengo la kupata uzoefu wa namna TSC inavyotekeleza majukumu yake katika kuhudumia walimu.

Ujumbe huo ulipokelewa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na kisha kufanya kikao na Menejimenti ya TSC ambapo pamoja na mambo mengine Mwl. Nkwama aliwaeleza wataalam hao kuwa Tume hiyo imeanzishwa kwa Sheria Sura 448 kwa lengo la kusimamia walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma Tanzania Bara.

“Tume yetu inasimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu. Tume hii inahusika na mwalimu tangu anapoingia kazini hadi anapostaafu kwa maana tunashughulika na ajira yake, tunamthibitisha kazini, tunampandisha cheo, tunambadilishia cheo pale anapojiendeleza kielimu na kutimiza vigezo, tunatoa kibali cha kustaafu lakini pia tunasimamia nidhamu na maadili yake,” alisema Katibu huyo.

Nkwama aliongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria hiyo, TSC ina ofisi katika wilaya zote 139 za Tanzania Bara ambapo ofisi hizo ndizo zinazomhudumia mwalimu moja kwa moja jambo ambalo limesaidia kurahisisha mwalimu kupata huduma.

Aliongeza kuwa TSC kwa kushirikiana na Mamlaka zingine imesaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa njia mbalimbali ikiwemo kuanzisha Mfumo wa Teachers’ Service Commission Management Information System (TSCMIS) ambao unamfanya mwalimu kuwasilisha changamoto zake kwa kutumia simu yake ya mkononi bila kutoka kwenye kituo chake cha kazi.

Kwa upande wake, kiongozi wa ujumbe huo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Bi. Mtumwa Iddi Hamad alimshukuru Katibu



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akikabidhi nyaraka mbalimbali za TSC kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bi. Mtumwa Iddi Hamad wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipotembelea TSC Februari 12, 2024.

wa TSC pamoja na Menejimenti ya Tume kwa kukubali kuwapokea na kuwapa uzoefu wa namna kazi zinavyofanyika katika chombo hicho cha kuhudumia walimu.

Alieleza kuwa Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuanzisha chambo cha kusimamia walimu tofauti na sasa ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo inayosimamia walimu moja kwa moja.

“Tumeangalia na kuona kuwa ninyi mmepiga hatua na mnafanya vizuri katika kusimamia utumishi wa walimu. Kwetu walimu ni wengi kuliko watumishi wengine wa umma, na tumegundua kuwa wizara inabeba mzigo mkubwa kitu ambacho kinasababisha usimamizi wa walimu kutofanyika kwa ufanisi. Hivyo tunakusudia kuanzisha Tume kama yenu na tumeona kuna mengi ya kujifunza kutoka kwenu kabla hatujaanzisha,” alisema Mkurugenzi huyo.

Wataalam wengine waliombatana na Bi. Mtumwa Iddi Hamad ni Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Bi. Maimuna Fadhi Abass na wanasheria wawili Bw. Massoud Haji na Bw. Said Malik Juma wote kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Ujumbe huo unatarajiwa kutembelea Ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino Februari 13, 2024 kwa lengo la kupata uzoefu wa namna ofisi za wilaya zinavyotekeleza majukumu yake.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na Wataalam kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ofisini kwake jijini Dodoma, Februari 12, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza katika kikao kilichokutanisha Menejimenti ya TSC na ujumbe wa wataalam kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Februari 12, 2024 katika Ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.




Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bi. Maimuna Fadhi Hamad akizungumza na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipotembelea TSC Februari 12, 2024.

Wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar, Bi. Maimuna Fadhi Abass (katikati), Massoud Haji (wa kwanza kulia) na Said Malik Juma wakiwa katika kikao na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wataalam (TSC) hao walipotembelea TSC Februari 12, 2024.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)



BURIANI


Ali Hassan Mwinyi

Rais Mstaafu wa Jamhuri ya
Muungano wa Tazanaia

1925 – 2024



www.tsc.go.tz



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania

MCHENGERWA AZINDUA MFUMO WA UFUNDISHAJI MUBASHARA (SMART CLASSES)



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akizungumza wakati wa uzinduzi wa majaribio ya mfumo wa ufundishaji mubashara (Smart Classes) Februari 7, 2024 jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

SERIKALI imeanza majaribio ya mfumo wa ufundishaji mubashara ambao mwalimu mmoja anaweza kufundisha wanafunzi wa nchi nzima kwa wakati mmoja.

Mfumo huo ambao kwa sasa unafanyiwa majaribio kwa baadhi ya shule za mikoa miwili ya Pwani na Dodoma, unamwezesha mwalimu kutoka kituo kimoja kufundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja wakiwa mikoa tofauti.

Utaratibu huo unaleta tafsiri ya kwamba mbali na kurahisisha utendaji kazi, pia ni njia mojawapo ya kukabiliana na uhaba wa walimu, hasa wa masomo ya



Wanafunzi wakiwa darasani wakati wa uzinduzi wa majaribio ya mfumo wa ufundishaji mubashara (Smart Classes) Februari 7, 2024 jijini Dodoma.


sayansi shuleni.

Wakati Serikali inaendelea na majaribio ya mfumo huo, wanafunzi wa Shule ya Sekondari

ya Dodoma wamesema mfumo huo utawasaidia kupata uelewa kwa wepesi na kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)



SALAAM ZA POLE

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu,
Menejimenti na Watumishi wote; tunaungana
na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutoa salamu
za pole kwa Familia, Ndugu, Jamaa, Marafiki
na Watanzania wote kufuatia kifo cha Rais wa
Awamu ya Pili **Mhe. ALI HASSAN MWINYI**

Inna lillahi wa inna ilaihi rajjiun!



www.tsc.go.tz



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania

WATAALAM WA ELIMU KUTOKA ZANZIBAR WATEMBELEA OFISI ZA TSC CHAMWINO

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Wataalam wa elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wameendelea na ziara ya kutembelea Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa lengo la kupata uzoefu wa namna Tume hiyo inavyotekeleza majukumu yake katika kuhudumia walimu.

Februari 13, 2024 wataam hao walitembelea Ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino ambapo walipokelewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Chamwino, Bi. Paulina Kanumba ambaye alishirikiana na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Dodoma, Bi. Leticia Mwakasitu kutoa ufafanuzi wa namna Ofisi za Wilaya zinavyofanya kazi.

Akizungumzia masuala la Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bi. Kanumba alieleza kuwa TSC ngazi ya Wilaya inapokea barua na idadi ya majina ya walimu wa ajira mpya kutoka kwa mwajiri, kusimamia ujazaji wa mikataba ya kazi ya walimu hao, kuwasajili na kuwapatia barua za ajira zenye masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

“TSC ngazi ya Wilaya ina jukumu la kuthibitisha kazini walimu wa ajira mpya baada ya miezi tisa (9) hadi 12 endapo wamemudu majukumu waliyopangiwa. Pia, tunawapandisha vyeo walimu kwa mujibu wa miongozo na taratibu zilizopo. Upandaji wa yeo wa walimu unategemea uwepo wa ikama, utendaji kazi, muda wa kutumikia cheo kimoja na bajeti iliyoidhinishwa. Pia, walimu wanaojiendeleleza kielimu tunawabadilishia kazi kwa mujibu wa taratibu,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa sheria, mwalimu anayefukuzwa kazi anaweza kuomba kurudi kuajiriwa tena baada ya kutumikia adhabu yake kwa kipindi kisichopungua miezi 12, hivyo ofisi za wilaya zina jukumu la kuwasilisha kwa TSC Makao Makuu mapendekezo ya walimu wanaoomba kuajiriwa tena.

Vilevile, alieleza kuwa Ofisi ya Wilaya ina jukumu la kutoa vibali vya kustafu kazi ya ualimu huku akifafanua kuwa kuna aina tatu za kustaaifu ambazo ni kustaaifu kwa hiari (baada ya kufikisha umri wa miaka 55 na kabla ya kufikisha miaka 60), kustaaifu kwa lazima (umri wa miaka 60) na kustaaifu kwa ugonjwa.

Alihitimisha kwa kuwaelezea wageni hao kuwa ofisi za Tume ngazi ya Wilaya zina jukumu la kuandaa TANGE za walimu kwa kuzingatia ukubwa wa vyeo kazini kwenye kada husika ambazo ni astashahada, stashahada na shahada.

Akizungumzia masuala ya Nidhamu kwa Walimu, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Dodoma, Bi. Leticia Mwakasitu aliwaelezea wataalamu hao



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Fatuma Muya akitoa neno la ukaribisho katika kikao kilichowakutanisha wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar na watumishi wa TSC kwa lengo la kuwapatia wataam kutoka Zanzibar uelewa na namna TSC ngazi ya Wilaya inavyoendesha shughuli zake. Kikao hicho kilifanyika Februari 13, 2024 katika ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino.

kuwa TSC inatoa adhabu kwa walimu wanaokiuka maadili ya kazi yao ambapo katika ngazi ya shule Mkuu wa Shule/ Mwalimu Mkuu amepewa mamlaka ya kushughulikia makosa mepesi na Ofisi za Wilaya zinashughulikia makosa mazito.

“Makosa mepesi ni kama utoro usiozidi siku tano, kuchelewa kazini na uzembe kazini ambapo adhabu zake ni pamoja na onyo na karipio. Makosa mazito yanashughulikiwa na Kamati ya Wilaya, makosa hayo ni pamoja na utoro unaozidi siku tano, wizi, rushwa, ubadhirifu, ugomvi na uchonganishi. Adhabu za makosa mazito ni kushushwa cheo, kuzuia nyongeza ya mshahara na kufukuzwa kazi,” alisema Mwakasitu.

Hata hivyo, alifafanua kuwa TSC imeweka nguvu zaidi katika kutoa elimu kwa walimu ili wajiepushe na tabia zinazokwenda kinyume na maadili ya kazi hiyo.

Kwa upande wake, kiongozi wa ujumbe huo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Bi. Mtumwa Iddi Hamad alishukuru kwa maelezo yaliyotolewa na kueleza kuwa yatawasaidia katika kuanzisha chombo cha kusimamia walimu kwa upande wa Zanzibar.

“Kwa niaba ya wenzangu, ninawashukuru sana kwa namna ambavyo mmetupokea na kutufahamisha taratibu mbalimbali za kusimamia utumishi wa walimu. Tumejifunza mengi ambayo yatatusaidia kuandaa chombo chetu ili kuleta maendeleo zaidi katika Sekta ya Elimu,” alisema.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Chamwino, Paulina Kanumba akitoa ufafanuzi juu ya masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu kwa wataalam wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Februari 13, 2024 katika Ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Dodoma, Leticia Mwakasitu akitoa ufafanuzi juu ya masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu kwa wataalam wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Februari 13, 2024 katika Ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino.

Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bi. Mtumwa Iddi Hamad akichangia mada wakati wa kikao kilichowakutanisha wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar waliofanya ziara TSC kwa lengo la kupata uzoefu wa namna Tume hiyo inavyofanya kazi. Kikao hicho kilifanyika Februari 13, 2024 katika ofisi za TSC Wilaya ya Chamwino.



Washiriki wa kikao cha wataalam wa elimu kutoka Zanzibar na TSC kilichofanyika Februari 13, 2024 katika Ofisi za TSC Chamwino wakikwa kwenye kikao hicho.



Washiriki wa kikao cha wataalam wa elimu kutoka Zanzibar na TSC kilichofanyika Februari 13, 2024 katika Ofisi za TSC Chamwino wakizwa kwenye kikao hicho.



Picha ya pamoja kati ya kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watumishi wa TSC Makao Makuu na TSC Wilaya za Chamwino na Dodoma wakati ujumbe wa wataalam wa elimu kutoka Zanzibar alipotembelea ofisi za TSC Chamwino Februari 13, 2024.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Kheri ya
SIKU40
ZA MFUNGO WA KWARESMA

TSC MISSENYI YAWAJENGEA UWEZO WALIMU WA KATA YA MUTUKULA NA KYAKA

Na Mwandishi wetu – Missenyi.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Missenyi, Februari 15 na 16, 2024 ili wajengea uwezo Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Kata ya Mutukula na Kyaka juu ya Sheria Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu ili walimu hao watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi.



Mafunzo kwa walimu wa Kata ya Mutukula na Kyaka yakiwa yanaendelea.

TSC MISSENYI YAWAJENGEA UWEZO WALIMU WA KATA YA MUTUKULA NA KYAKA



Mafunzo kwa walimu wa Kata ya Mutukula na Kyaka yakiwa yanaendelea.

SERIKALI KUENDELEA KUONGEZA NGUVU KATIKA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KUKABILIANA NA UPUNGUFU WA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Serikali imesisitiza kuendelea kuweka nguvu kwenye matumizi ya teknolojia katika kutoa elimu shuleni ikiwa ni moja ya njia za kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu nchini.

Hayo yamesemwa Februari 12, 2024 na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde wakati alipotembelewa na ujumbe wa wataalamu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapindinduzi ya Zanzibar ambao wamefanya ziara Tume ya Utumishi wa Walimu kwa lengo la kujifunza namna Tume hiyo inavyotekeleza majukumu yake.

Dkt. Msonde alisema Serikali chini ya Utawala wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya jitihada

mbalimbali za kuboresha elimu ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu kama inavyohitajika.

“Kwa sasa tumeanza majaribio ya matumizi ya teknolojia ya ufundishaji inayowezesha Mwalimu kutoka kituo kimoja kufundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja wakiwa katika maeneo mbalimbali. Tumeanza majaribio haya katika Mikoa miwili ya Pwani na Dodoma na kwa kweli matokeo yake ni mazuri na wanafunzi wanafurahia,” alisema Dkt. Msonde.

Aliongeza kuwa, “kupitia teknolojia hiyo mwalimu anaona wanafunzi wake wote katika maeneo mbalimbali, anaweza kuuliza swali na mwanafunzi akanyoosha mkono na kujibu, yaani ni kama vile mwalimu yupo hapo hapo.”

Naibu Katibu Mkuu huyo aliongeza kuwa mbali na mfumo huo kurahisisha utendaji kazi kwa walimu, ni moja ya njia za

kukabiliana na upungufu wa walimu hususan wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Ameongeza kuwa katika kuendelea jitihada hizo, Waziri wa Nchi OR – TAMISEMI, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) tayari ameagiza kutengwa kwa bajeti ili kuwezesha upatikanaji wa angalau darasa moja kwa kila Mkoa na kila Halmashauri katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Pamoja na hayo, Dkt. Msonde alieleza kuwa TSC imeendelea kusimamia masuala ya utumishi wa walimu kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu ambapo hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kumaliza malalamiko ya walimu.

“Kama mna mpango wa kuanzisha chombo cha kushughulikia masuala ya walimu kama TSC, ninaamini mtapata mengi ya kujifunza na hivyo mtapata mwanga mzuri wa kuanzisha chombo kitakachosaidia upatikanaji wa huduma kwa walimu,” alisema Dkt. Msonde.

Kwa upande wake kiongozi wa ujumbe huo ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Bi. Mtumwa Iddi Hamad alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar ndiyo inayoshughulika moja kwa moja na usimamizi wa walimu kitu ambacho kinaleta changamoto katika usimamizi stahiki kwa walimu.

“Kutokana na hali hiyo Serikali ya Zanzibar inakusudia kuanzisha chombo maalum cha kushughulikia masuala ya walimu, hivyo tumekuwa kujifunza kwa TSC ili kupata uzoefu wa namna inavyosimamia walimu huku Tanzania Bara,” alisema Mkurugenzi huyo.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde akizungumza na Wataalamu wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na wataalamu wengine kutoka TSC waliofika ofisini kwa Naibu Katibu Mkuu huyo jijini Dodoma, Februari 12, 2024.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde akizungumza na Wataalamu wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na wataalamu wengine kutoka TSC waliofika ofisini kwa Naibu Katibu Mkuu huyo jijini Dodoma, Februari 12, 2024.



Kiongozi wa ujumbe wa wataalamu wa elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Wizara hiyo, Bi. Mtumwa Iddi Hamad akitoa neno la shukrani kwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani), wakati ujumbe huo ulipomtembelea Naibu Katibu Mkuu huyo ofisini kwake jijini Dodoma Februari 12, 2024.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akitoa utambulisho wa wageni alioawaongoza kumtembelea Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde ofisini kwake jijini Dodoma, Februari 12, 2024.



Wataalamu wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na TSC wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani) Februari 12, 2024 jijini Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (wa nne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto), Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wa Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar, Bi. Mtumwa Iddi Hamad (wa nne kutoka kushoto) na wataalamu wengine kutoka TSC na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar katika ofisi za Naibu Katibu Mkuu huyo jijini Dodoma Februari 12, 2024.

KAMATI YA BUNGE YAPONGEZA TEKNOLOJIA MPYA YA UFUNDISHAJI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetembelea Shule ya Sekondari Dodoma kujionea majaribio ya Mfumo wa Ufundishaji Mubashara 'Live Teaching' ambao unawezesha Wanafunzi wa Shule nyingine nchini kuunganishwa na Mwalimu anayefundisha katika Shule ya Sekondari Kibaha Mkoani Pwani.

Akizungumza baada ya kujionea mfumo huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Denis Londo

alisema wameridhishwa na mfumo huo huku akiipongeza Serikali kwa kuja na teknolojia hiyo ambayo inakwenda kukuza kiwango cha elimu nchini.

"Niipongeze Serikali yetu inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika Sekta ya Elimu, tumejionea shule nyingi zikijengwa, uwekezaji wa elimu bila malipo hadi kidato cha sita na sasa teknolojia hii ya Wanafunzi wa shule nyingine kushiriki kipindi cha masomo na wenzao waliopo Kibaha Sekondari." Alisema Mwenyekiti huyo.

"Rai yetu kama Kamati ni kuitaka

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuusimamia kikamilifu mfumo huu ili uweze kuleta tija kwa Wanafunzi wetu nchini. Lakini niwatake Wanafunzi hawa wanaonufaika na mfumo huu kuutumia kikamilifu ili waweze kufaidika nao kwenye masomo yao na kupata matokeo mazuri." Alisema Mhe. Londo.

Naye, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde, alisema wamepokea maelekezo ya Kamati hiyo na kwamba watahakikisha mfumo huo unatumika ipasavyo kama ilivyokusudiwa na kuwa wenye manufaa kwa Wanafunzi nchini.



MATUMIZI YA TEHAMA SEKTA YA ELIMU KUIMARISHWA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amekutana na wawakilishi wa Kampuni ya Teknolojia ya HUAWEI Tanzania wakiongozwa na Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni hiyo Bw. Eric Yang Jijini Dodoma.

Viongozi hao walijadili kuhusu ushirikiano wenye lengo la kuimarishaji ufundishaji na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ya Elimu.





Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote 184 nchini wakishirikiana na Maafisa kutoka Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na TAMISEMI wakiendelea na kazi maalum ya kuchambua na kuhakiki taarifa za walimu kwa lengo la kubainisha walimu wenye changamoto na malalamiko ili Serikali izeze kuchukua maamuzi na hatua stahiki ya kumaliza kabisa changamoto hiyo. Kazi hiyo ilifanyika hivi karibuni fjijini Dodoma.





Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote 184 nchini wakishirikiana na Maafisa kutoka Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na TAMISEMI wakiendelea na kazi maalum yakuchambua na kuhakiki taarifa za walimu kwa lengo la kubainisha walimu wenye changamoto ili Serikali izeze kuchukua maamuzi na hatua stahiki ya kumaliza kabisa changamoto hiyo. Kazi hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Dodoma.





Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri zote 184 nchini wakishirikiana na Maafisa kutoka Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na TAMISEMI wakiendelea na kazi maalum yakuchambua na kuhakiki taarifa za walimu kwa lengo la kubainisha walimu wenye changamoto ili Serikali iweze kuchukua maamuzi na hatua stahiki ya kumaliza kabisa changamoto hiyo. Kazi hiyo ilifanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.

WASIMAMIZI WA ELIMU WILAYA YA NACHINGWEA WAKUTANA KUJADILI MAENDELEO YA ELIMU

Na Mwandishi wetu – Nachingwea.

Wasimamizi wa Elimu katika Wilaya ya Nachingwea walifanya kikao Februari 14, 2024 kujadili masulala mbalimbali ya elimu katika Wilaya hiyo.

Kikao hicho kiliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo na kuhudhuriwa na Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Nachingwea, Afisa Elimu Msingi na Sekondari, Mthibiti Ubora wa Shule, pamoja na maafisa wengine kutoka idara ya Elimu katika Halmashauri hiyo.



Kikao cha Wasimamizi wa Elimu Katika Wilaya ya Nachingwea kikiwa kinaendelea.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi zawadi Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bi. Mtumwa Iddi Hamad wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipohitimisha ziara yao TSC Februari 13, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi zawadi Mkuu wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bi. Maimuna Fadhi Abass wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipohitimisha ziara yao TSC Februari 13, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi zawadi Mwanasheria kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bw. Said Malik Juma wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipohitimisha ziara yao TSC Februari 13, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi zawadi Mwanasheria kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bw. Massoud Haji wakati ujumbe wa wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipohitimisha ziara yao TSC Februari 13, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wataalam wa Elimu kutoka Zanzibar walipohitimisha ziara yao TSC Februari 13, 2024. Pichani, wa kwanza kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya.

IMARISHENI ULINZI WA VIFAA VIPYA VYA TEHAMA MASHULENI – WAZIRI MCHENGERWA

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, amewaelekeza Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha wanaimarisha ulinzi na kufikisha kwenye vituo teule vifaa vya TEHAMA vilivyogawiwa kwa vituo zaidi ya 800 kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST).

Mchengerwa aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa Uzinduzi wa Ugawaji wa Vifaa vya TEHAMA kwa Vituo vya Walimu na Shule za Awali na Msingi uliofanyika Jijini Dodoma.

“Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri imarisheni ulinzi na usalama katika shule zitakazopokea vifaa vya TEHAMA na ndani ya siku tatu vifaa hivi viwe vimekabidhiwa kwa mikoa husika.” Alisema Waziri Mchengerwa.

Aidha, aliwataka kuhakikisha

shule zinazopelekwa vifaa hivyo zisibadilishwe isipokuwa labda kwa kibali maalumu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mhe. Mchengerwa aliwataka watendaji hao kusimamia matumizi ya vifaa hivyo ili kuleta mapinduzi makubwa katika eneo la ujifunzaji na ufundishaji na kwamba yeye mwenyewe atapita kukagua utekelezaji wake lakini pia matarajio ya Serikali ni kuongeza vifaa zaidi ili shule zote ziweze kufikiwa.

Waziri Mchengerwa alimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za dhati katika kuboresha sekta ya elimu nchini.

Kwa upandewake Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ndg. Franklin Rwezamula, aliipongeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kununua vifaa vya TEHAMA kupitia Mradi wa Kukuza Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) kwa lengo la kuimarisha Vituo vya Walimu (TRC) na Shule zilizoteuliwa kama sehemu muhimu ya kutolea

Mafunzo endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) na kuwezesha zoezi la Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Wanafunzi ambao watatumia vituo hivyo zaidi ya 800.

Vilevile, alisema Wizara ya Elimu itaendelea kutoa ushirikiano katika Utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 ambayo sasa ipo katika utekelezaji wake kwenye mitaala iliyoboreshwa hapa nchini.

Akitoa shukrani zake kwa Serikali Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mtemi Mazengo, Valikaeli Mfinanga, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kujifunzia masomo ya sayansi kwa vitendo kwa kuwa vitawasaidia kuwa na ukurasa mmoja na Wanafunzi wengine ndani na nje ya Tanzania na kupata ujuzi na maarifa mbalimbali.

Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) mpaka sasa umejenga Shule Mpya za Awali na Msingi 302, Ofisi za Walimu, Mabweni na Matundu ya Vyoo.



PROF. CAROLYNE NOMBO AONGOZA KIKAO KATI YA WATAALAMU KUTOKA UNICEF NA WIZARA KUJADILI MASUALA MBALIMBALI YA UBORESHAJI WA ELIMU NCHINI

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyn Nombo, ameongoza kikao kati ya Wataalamu kutoka UNICEF na Wizara kujadili masuala mbalimbali ya uboreshaji wa elimu nchini.

Kikao hicho ambacho kilifanyika Jijini Dodoma pamoja na mambo mengine kilijadili juu ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kidijitali, Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2024 Toleo la 2023 na rasilimali zilizopo kwa ajili ya utafiti, ufuatiliaji na tathmini katika Sekta ya Elimu.

Akizungumza katika kikao hicho Katibu Mkuu huyo alisema kuwa Wizara ipo katika mchakato wa kuwa na mwongozo katika suala la kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundishia na kujifunzia ili kuwezesha utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa.



SERIKALI INAENDELEA KUONDOA VIKWAZO VYA KUPATA ELIMU KWA KUTOA ELIMU BILA ADA

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Serikali inaendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kuondoa vikwazo vya kupata elimu kwa kutolewa kwa elimu ya msingi bila ada, kuifanya elimu ya lazima kuwa miaka 10 na kutekeleza programu zenye lengo la kuwafikia Watanzania waliokosa fursa za elimu.

Hayo yalielezwa hivi karibuni Bungeni Jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omari Kipanga, wakati akijibu swali la Mhe. Taska Restituta Mbogo (Viti Maalum), aliyetaka kufahamu mikakati ya Serikali ya kuhakikisha Watanzania wote wanajua kusoma na kuandika ambapo aliongeza kuwa mikakati hiyo ni Elimu ya Watu Wazima na ujifunzaji endelevu, utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kisomo pamoja na kutoa fursa kwa Wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali kurudi shuleni na kuendelea

na masomo (re-entry program) kupitia Waraka Na. 2 wa mwaka 2021.

Mhe. Kipanga aliongeza kuwa Serikali inaendelea kuboresha huduma za maktaba nchini katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shule ikiwa ni pamoja na Maktaba Mtandao ili kuwawezesha Watanzania wengi zaidi katika maeneo mbalimbali kupata huduma ya kujisomea huko waliko na kwamba itaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Elimu ya Wazima kwa lengo la kuongeza fursa kwa Watanzania wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Watu Wazima.

Naibu Waziri huyo alisema kulingana na taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 nchini Tanzania kwa kufikia kiwango cha asilimia 83 cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa watu wazima yaani miaka 15 na kuendelea ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.3 toka asilimia 78.1 ya Sensa ya Mwaka 2012.



SIMAMIENI MAGARI YALIYOTOLEWA KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA ELIMU – WAZIRI MCHENGERWA

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, amewaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanasimamia matumizi sahihi ya magari mapya 13 yaliyotolewa na Serikali kuwa yanaleta tija ya kuwahudumia Watumishi na Wananchi.

Mheshiwa Mchengerwa aliyasema hayo hivi karibuni Jijini Dodoma katika Kituo cha Jakaya Kikwete alipokuwa akifungua Kikao Kazi cha Kushughulikia Changamoto za Upandishaji wa Vyeo na Kubadilisha Kada kwa Walimu.

Waziri Mchengerwa pia aliwataka Viongozi hao kote nchini kuhakikisha katika taarifa zao za utendaji kazi wa kila mwezi anapata taarifa ya utendaji kazi wa Maafisa Elimu na Idara ya Afya ili kuona kama magari yaliyotolewa kwa shughuli za ufuatiliaji na utatuzi wa kero za Wananchi zinafanyiwa kazi kwa wakati pamoja na Maafisa Elimu kwenda vijijini kutatua kero za Walimu.

“Maafisa Elimu fanyeni mikutano na Walimu, nendeni mshuke vijijini mkatatue kero na changamoto za Walimu mara moja na zile zilizo nje ya uwezo wenu kazileteni kwetu.” Alisema Mheshimiwa Mchengerwa.

Vilevile, Waziri huyo alifanya zoezi la kugawa magari 13 yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 1.8 yatakayosaidia ufuatiliaji wa masuala ya Elimu Msingi katika Halmashauri 13 kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) na kuwaelekeza Viongozi wa Mikoa na Wilaya kufuatilia matumizi sahihi

ya magari hayo.

Katika hatua nyingine Waziri Mchengerwa alisema Serikali ilisaini Mradi Mpya na Wadau wa GPE ambao una Afua za Kutatua Changamoto za Walimu nchini unaojulikana kama ‘Teacher Support Programme - (TSP)’ yenye thamani ya Shilingi Bilioni 264 ambao umeanza katika Mwaka wa Fedha wa 2023/ 2024 ikiwa ni matunda ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshiwa Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anaimarisha mahusiano ya Kimataifa na nchi na Wadau mbalimbali wa maendeleo.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (USEMI). Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, alisema magari yaliyotolewa na Programu ya Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) yatasaidia kuhamasisha utendaji kazi na utekelezaji wa kitaaluma

hasa maeneo ya pembezoni kwani yatasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Rosemary S. Senyamule, akitoa maelezo ya awali kabla ya Hotuba ya Mgeni Rasmi aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo ya Serikali na alimshukuru Mhe. Mchengerwa kwa kuwapatia changamoto ya kwenda kufuatilia Miradi ya Maendeleo na Kero za Walimu kwani maelekezo hayo yamezaa matunda kwa kuwa ufanisi unaonekana kwa kukamilika miradi ya maendeleo na kuongezeka kwa Ufaulu wa Wanafunzi na sasa kama mkoa wameandaa Mpango Mkakati wa Elimu wa Mkoa na ataukabidhi kwake rasmi.

Naye, Peter Fusi, Afisa Elimu (Msingi), Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, alitoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwapatia gari kupitia Programu ya GPE kwani yeye ndiye sauti yao kwa Wadau wa Maendeleo na sasa wataweza kufika maeneo korofi kama yale yanayozunguka Mto Ruaha na Bwawa la Mtera.



SERIKALI KUENDELEA KUTOA KIPAUMBELE KWA WANAOSOMA MASOMO YA SAYANSI

Na. Mwandishi Wetu – Arusha.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema Serikali inaendelea kutoa kipaumbele kwa wanaosoma Masomo ya Sayansi ikiwemo kutoa ufadhili wa masomo hayo ili kuongeza hamasa kwa Vijana wa Kitanzania wakiwemo Wasichana kupenda kusoma masomo hayo.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo hivi karibuni Mkoani Arusha katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi, ambapo alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuwekeza katika mazingira mazuri kwa ajili ya vijana kupata fursa mbalimbali katika Nyanja za Sayansi za masomo na kuendeleza ubunifu ili kuendana na kasi ya teknolojia duniani na hata soko la ajira ndani na nje ya nchi.

“Taifa lina upungufu wa Wanasayansi na hasa Wanawake na Wasichana, kwasababu ni wachache wanaosoma Masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu (STEM) hivyo tutaendelea kuhamasisha Wasichana wengi zaidi kupenda na kujiunga na masomo hayo.” Alisema Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa ili Taifa liendeleo linahitaji Wanasayansi. Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wadau mbalimbali wataendelea kufungua fursa na kuweka mazingira sahihi ya Ujifunzaji katika Sayansi.

Alibainisha kuwa Serikali inatekeleza baadhi ya afua ili kuongeza idadi ya Wataalam Wanawake wa Sayansi, ikiwa

ni pamoja na kutoa ufadhili wa masomo ikiwemo Samia Scholarship na Mikopo, kujenga Shule za Sekondari Maalum za Sayansi za Wasichana kila Mkoa, kuimarisha Mafunzo ya Ualimu wa Sayansi, kufanya Mapitio ya Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kupitia Mitaala Mipya kutoa msukumo katika masuala ya kuwezesha Wanafunzi kuwa na fikra tunduizi na kutoa kipaumbele katika Somo la TEHAMA ambapo itandaa Wanasayansi wa kuwezesha kwenda sambamba na mapinduzi ya nne ya viwanda.

Mkurugenzi wa Elimu Endelevi kutoka Taasisi ya STEM katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Dkt. Leonard Mwalongo, aliishukuru Serikali kwa kutoa Ufadhili wa Masomo ya Sayansi kwa Wasichana waliopungukiwa sifa za moja kwa moja za kujiunga na Vyuo Vikuu katika Kozi za Sayansi kupitia ‘Foundation Program’ ya Mwaka mmoja inayotolewa na OUT.

“Ufadhili huu ni asilimia mia moja unatolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kwa miaka 5. Tunatarajia kufadhili Wanafunzi 1,000 ambapo kila mwaka Wanafunzi 200 watanufaika.” Alisema Dkt. Mwalongo.

Akiwasilisha mada Mzungumzaji Mkuu, Prof. Verdiana Masanja, alisema kuwa hapa Tanzania ni asilimia 12 pekee ya Wanawake ambao wapo katika Uongozi wa Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu (STEM), na kwamba ni wakati muafaka kuwahimiza Wasichana na Wanawake pamoja na kuweka mazingira kwa ajili ya kusaidia ukuaji wao katika masuala ya Uongozi, Taaluma na Ujasiriamali bila kusahau kuwaandaa kuingia katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yakisukumwa na Teknolojia Mpya ikiwemo AI (Artificial Intelligence) na IOT (Internet Of Things).





TUNAHITAJI WALIMU BORA, MAHIRI KATIKA KUFUNDISHA NA KULINDA MAADILI – PROF. MKENDA

Na. Mwandishi Wetu – Tanga.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia prof. Adolf Mkenda amesema Taifa linahitaji Walimu bora na mahiri katika kufundisha pamoja na uwezo wa kukaa na kuwalea vizuri watoto wa Kitanzania ili wafikie malengo yao na kusaidia nchi katika nyanja mbalimbali.

Waziri Mkenda alitoa rai hiyo hivi karibuni Mkoani Tanga wakati akifungua Mafunzo ya Kitaifa ya Kuwajengea Uwezo Walimu Wakuu wa Shule za Msingi wapatao 347, kutoka Wilaya ya Korogwe Mji, Korogwe Vijijini na Lushoto kuhusu Uongozi, Usimamizi wa Shule na Utawala Bora yaliyofanyika katika Chuo cha Ualimu Korogwe.

Prof. Mkenda alieleza kuwa mageuzi ya Elimu ndio agenda kubwa Duniani, na kwamba tayari Serikali ilishaanza kufanyia kazi mageuzi hayo ili kuendana na wakati pamoja na kukidhi mahitaji ya sasa na baadae ya Taifa na Kitaifa.

“Hatutaki Ualimu uvamiwe, tunahitaji kuulinda pamoja na kuwasaidia Walimu kujiendeleza Kitaaluma. Hivyo, kwenye Sera sasa hivi itakuwa ni lazima anayemaliza Chuo cha Ualimu aende akafanye mazoezi ya kazi kwa mwaka mmoja apimwe ili aweze kuhitimu kama kada zingine zinavyofanya.” Alisema Waziri Mkenda.

Alisema azma ya Serikali ni kurudisha heshima ya Ualimu na kuhakikisha tunapata Walimu wenye sifa stahiki, bora, wenye uwezo na umahiri wa kufundisha na kulea watoto kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania.

Aidha, alibainisha kuwa Serikali itaendelea kufanya juhudi kuhakikisha Walimu wanathaminiwa katika kutenda kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu mbalimbali, kununua vifaa ikiwemo vishkwambi na kuweka mazingira rafiki katika utekelezaji wa majukumu yao.

Prof. Mkenda aliongeza kuwa mpaka sasa Walimu wamefanya kazi kubwa, na kwamba bado kuna kazi kubwa zaidi inawahitaji kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

“Tunawaheshimu sana Walimu wote, na ni ukweli usiopingika kwamba Walimu ndio tegemeo letu kubwa sana hapa nchini. Mmechangia kwa kiasi kikubwa mageuzi makubwa yanayofanyika katika



Elimu yetu, bila nyie hatuna elimu.” Alieleza Mkenda.

Nae Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Dkt. Siston Masanja, alisema mafunzo hayo yanatekelezwa kwa awamu ya pili, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi (BOOST) kupitia afua namba 8 ambayo ADEM ilipewa jukumu na Wizara ya Elimu, kuendesha mafunzo kwa Walimu Wakuu 17,000 nchini hasa kwa Tanzania Bara.

Alibainisha kuwa awamu ya kwanza ya mafunzo hayo ilitekelezwa kati ya mwezi Septemba na Oktoba, 2023 ambayo ilihusisha kati ya Walimu Wakuu 4,522 kutoka Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Njombe, Songwe, Morogoro, Dodoma na Mkoa wa Mara.

“Awamu hii jumla ya Walimu Wakuu 4,620 kutoka Mikoa sita ya Tanzania Bara watapatiwa mafunzo ikiwemo kutoka Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Kigoma, Mtwara, Simiyu na Mbeya. Zoezi hili litaendelea kwa Mikoa iliyobaki.” Alisema Dkt. Masanja.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Mhe. William Mwakilema, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya Elimu kuanzia Elimu ya Awali mpaka Vyuo, na kwamba imeendelea kuchagiza maendeleo katika Wilaya hiyo na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mafunzo hayo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kerenge Mlemwa iliyopo Korogwe Vijijini, Philipo Chombo aliahidi kutumia vema ujuzi na maarifa watakayoyapa katika kutekeleza majukumu yao kwa manufaa ya Wanafunzi na Jamii kwa ujumla.



WAZIRI SIMBACHAWENE AWAPONGEZA WALIMU MPWAPWA KWA KUFANYA VEMA KATIKA MITIHANI

**Na. Mwandishi Wetu –
Mpwapwa.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, amewapongeza Idara ya Elimu Sekondari ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kufanya vizuri katika Mtihamani wa Kidato cha Nne na kushika Nafasi ya Kwanza Kimkoa huku wakishika Nafasi ya Pili Kimkoa kwa matokeo ya Kidato cha Pili.

Kauli hiyo ameitoa hivi karibuni wakati alipokutana na ujumbe wa Walimu hao Bungeni

Jijini Dodoma ukiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mhe. George Fuime na Afisa Elimu Sekondari pamoja na Maafisa Elimu na Walimu Wakuu wa Sekondari 32 za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Alisema kila jambo linalotokea lina msingi wake na Msingi Mkuu ni Utendaji Mzuri na Ushirikiano katika kazi zote kwa kuangalia mazuri ya kila kitu na mazuri ya kila mtu.

“Kuangalia mazuri ya Wanafunzi, mazuri ya Walimu, na mazuri ya Viongozi yanasaidia katika kuweza kupata matokeo mazuri.” Alisema Mhe. Waziri

Kwa upande wake Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya

Wilaya ya Mpwapwa, Mwalimu Bernadetha Thomas, alisema Waziri aliwaalika baada ya kufanya vizuri katika Matokeo ya Kitaifa ya Mitihani ya Kidato cha Nne na Pili.

“Tumepanda kutoka asilimia 88 ambacho ni kiwango cha mwaka juzi mpaka asilimia 95 mwaka huu kwa Wanafunzi waliopata ufaulu wa Daraja la Kwanza mpaka Daraja la Nne kwa mwaka 2023 na mchango huu umechangiwa na Shule 11 za Kata.” Alisema Afisa Elimu Sekondari huyo.

Aidha, alisema; “Tumechukua ushauri wa Mhe. Waziri kama maelekezo kwetu kwa kuwa amekuwa akituongoza katika mabadiliko haya chanya katika Sekta ya Elimu kwa nyakati zote.”



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mhe. George Fuime (kushoto) akiwa na Maafisa Elimu na Walimu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa wakifuatilia Kikao cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Bunge la 12, Mkutano wa 14 Jijini Dodoma.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)